TANGAZO LA SERIKALI NA. 339 la tarehe 5/5/2023

SHERIA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetoleewa chini ya kifungu cha 29(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA LUSHOTO (LUSHOTO WSSA) YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana ni Amri ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Lushoto (Lushoto WSSA), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za maji safi na usafi wa mazingira za Lushoto WSSA zinarekebishwa kamazilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitakuwa na masharti yafuatayo:

(a) Mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023, LushotoWSSA itapaswa kuwasilisha uthibitisho kwa EWURA kwamba iliwataarifu wateja wake kuhusu Notisi mpyaya bei na kwamba iliwafahamisha ipasavyo wadau wake ikiwa ni pamoja na wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa kisiasa na wawakilishi wa taasisi za dini, juu ya mabadiliko ya bei;

(b) mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023 Lushoto WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa

biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

Sura ya 414 T.S. Na. 420 la mwaka 2021

(c) Lushoto WSSA itazingatia kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA, na kanuni ya 5 ya Kanuni za EWURA (Utaratibu wa Kukusanya Ada na Tozo) za kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(d) Lushoto WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei na ada zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(e) Lushoto WSSA itahakikisha kuwa wateja wote wasio na dira wanafungiwa dira za maji ifikapo tarehe 30 Juni 2023;

(f) Mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023, Mamlaka ya Maji Lushoto itaandaa na kutekeleza mpango wa kuwafikia wateja wote na kuwasilisha kwa EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(g) Lushoto WSSA itahakikisha taarifa zake za fedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuwasilisha taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa EWURA kila mwaka;

(h) Lushoto WSSA itashirikiana na Halmashauri ya Mji wa Lushoto ili kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka ifikapo tarehe 30 Juni 2023;

(i) Lushoto WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu;

(j) Lushoto WSSA, kila mwaka na kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hii; na

(k) Lushoto WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifazake za kifedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumwa

na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Lushoto WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji safi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa kwa Amri ya Bei Na. 11-014 la mwaka 2011 2011.

4. Amri hii inafuta Amri ya Bei ya mwaka 2011.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa

| Kundi la Wateja | 2021/22 | | Bei Zilizoidhinishwa (Shilingi kwaMitayaUjazo) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Matumizi | Bei za Sasa | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 1-15 | 3,000 Shs/mwezi | 800 | 900 | 1,000 |
| | 16-30 | 300 | | | |
| | 31-50 | 300 | | | |
| | >50 | 395 | | | |
| Taasisi | 1-20 | 8,000 Shs/mwezi | 1,150 | 1,350 | 1,360 |
| | 21-100 | 450 | | | |
| | >100 | 550 | | | |
| Biashara | 1-20 | 8,000 Shs/mwezi | 1,250 | 1,380 | 1,420 |
| | 21-100 | 455 | | | |
| | >100 | 560 | | | |
| Viwanda | 1-16 | 5000 Shs/mwezi | 1,290 | 1,400 | 1,500 |
| | 17-100 | 500 | | | |
| | >100 | 500 | | | |
| Magati | N/A | 1,000 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| Wastani | | 464 | 1,000 | 1,100 | 1,200 |

Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa |
|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 |
| Majumbani | 4,500 | 8,000 |
| Taasisi | 10,000 | 15,000 |
| Biashara | 9,500 | 20,000 |

Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 75,000 | 26,000 | | |
| Taasisi | 75,000 | 26,000 | | |
| Biashara | 75,000 | 26,000 | | |
| Viwanda | 75,000 | 26,000 | | |

Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(d))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Na. | Maelezo | Gharama (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | Kukarabati miundombinu ya chanzo cha maji cha Makunguru ifikapo Juni 2024 | - | 10.00 | - |
| | Kukarabati miundombinu ya chanzo cha maji cha Kamfa ifikapo Juni 2025 | - | - | 10.00 |
| | Kununua na kufunga dira kubwa 6 kwenye vyanzo vya maji vya Kwembago, Kwembago Makunguru, Kwembago Chamavita, Kamfa, Kindoi na Kibohelo ifikapo Juni 2023. | 6.00 | - | - |
| | Kujenga uzio kuzunguka vyanzo vya maji vya Kwembago na Kwembago Makunguru ili kulinda na kuzuia uingiaji wa watu wasioruhusiwa ifikapo Juni 2023. | 10.00 | - | - |
| | Kujenga uzio kuzunguka vyanzo vya maji vya | - | 10.53 | - |

*Tangazo La Serikali Na. 339 (Linaendelea)*

| Na. | Maelezo | Gharama (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | Kwembago Chamavita na Kamfa ili kulinda maji na kuzuia uingiaji wa watu wasioruhusiwa ifikapo Juni 2024 | | | |
| | Kujenga uzio kuzunguka vyanzo vya maji vya Kindoi na Kibohelo ili kuzuia uingiaji wa watu wasioruhusiwa ifikapo Juni 2025. | - | - | 15.08 |
| | Kujenga bomba kuu la usambazaji maji lenye urefu wa kilomita 1 na kipenyo cha milimita 63 kutoka tanki la kuhifadhi maji la Yoghoi hadi eneo la Yoghoi kufikia Juni 2024. | - | 25.00 | - |
| | Kujenga tanki la kuhifadhia maji lenye uwezo wa mita za ujazo 50 katika eneo la Kwamamoyo ifikapo Juni 2024 | - | 35.00 | - |
| | Kujenga bomba kuu la maji lenye urefu kilomita 1 aina ya HDPE la kipenyo cha milimita 75 (PN10) kutoka tanki la kuhifadhia maji la Mbura hadi eneo la Montessori ifikapo Juni 2025 | - | - | 32.00 |
| | Kujenga bomba kuu lenye urefu wa kilomita 1.5 aina ya HDPE la kipenyo cha milimita 75 (PN12.5) kutoka tanki la kuhifadhia maji la Mbura hadi tanki la kuhifadhia maji la Kwamamoyo ifikapo Juni 2024 | - | 46.00 | - |
| | Kujenga bomba kubwa lenye urefu wa kilomita 3.5 la kipenyo cha milimita 90 aina ya HDPE (PN10) kutoka Kindoi hadi Mbura ifikapo Juni 2025 | - | - | 44.00 |
| | Kukarabati bomba lenye urefu wa kilomita 1.2 la kipenyo cha milimita 75 aina ya HDPE (PN10) kutoka eneo la Irente hadi tanki la kuhifadhia maji la Yoghoi ifikapo Juni 2025 | - | - | 37.00 |
| | Kuongeza mita 500 za bomba la mtandao wa usambazaji wa maji la kipenyo cha milimita 63 aina ya HDPE (PN 10) eneo la Kialilo kufikia Juni 2023. | 12.00 | - | - |
| | Kuongeza mtandao wa bomba la usambazaji maji lenye kipenyo cha milimita 63 aina ya HDPE (PN 10) kwa mita 500 huko Kwesimu ifikapo Juni 2024. | - | 12.50 | - |
| | Kuongeza mtandao wa bomba la usambazaji maji lenye kipenyo cha milimita 63 aina ya HDPE (PN 10) kwa mita 500 huko Montessori kufikia Juni 2025 | - | - | 13.00 |
| | Kuongeza mtandao wa bomba la usambazaji maji lenye kipenyo cha milimita 63 aina ya HDPE (PN 10) kwa kilomita 1 katika eneo la Magamba (mita 500 mwaka wa fedha 2023/24 na mita 500 katika mwaka wa fedha 2024/25) | - | 12.50 | 13.00 |
| | Kubadilisha sehemu ya bomba la Kwembago urefu wa mita 500 na bomba aina ya HDPE (PN 10) lenye kipenyo cha milimita 90mm ifikapo Juni 2024 | - | 14.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba lenye urefu wa mita 250 kwa kutumia bomba aina ya HDPE (PN 10) yenye kipenyo cha milimita160 kwenye sehemu ya bomba la Kwembago (mita 100 katika mwaka 2023/24 na mita 150 kwa mwaka 2024/25 | - | 10.00 | 12.00 |
| | Kubadilisha sehemu ya mtandao wa bomba la Kamfa lenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE lenye kipenyo cha milimita 90 ifikapo Juni 2025 | - | - | 15.00 |

*Tangazo La Serikali Na. 339 (Linaendelea)*

| Na. | Maelezo | Gharama (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 250kwa kutumia bomba aina ya HDPE (PN 10) lenye kipenyo cha milimita 110, kwa bomba la Kamfa ifikapo Juni 2025 | - | - | 11.00 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 250kwa kutumia bomba aina ya HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita160 kwa sehemu ya bomba la Kibohelo ifikapo Juni 2025 | - | - | 20.00 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN10) zenye kipenyo cha milimita 110 kwa sehemu ya bomba la Kibohelo ifikapo Juni 2024 | - | 21.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa kilomita 1 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 12.5) zenye kipenyo cha milimita 90 (mita 300 kwa mwaka 2022/23, mita 300 kwa mwaka 2023/24 na mita 400 kwa mwaka 2024/25 eneo la Lushoto | 12.00 | 14.00 | 15.50 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bombza za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 75, huko Chakechake ifikapo Juni 2024 | - | 12.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 75, huko Chakechake Magesti ifikapo Juni 2025. | - | - | 12.00 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 250 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 63, huko Maguzoni ifikapo 2023 | 5.00 | - | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 50, huko Dochi ifikapo Juni 2023 | 7.00 | - | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 50, huko Chakechake ifikapo Juni 2024 | - | 7.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) wenye kipenyo cha milimita 50 huko Magamba Kosti ifikapo Juni 2025 | - | - | 7.00 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) na kipenyo cha milimita 32, huko Mabwawani ifikapo Juni 2023 | 5.00 | - | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) na wenye kipenyo cha milimita 32 eneo la Kitivo ifikapo Juni 2024 | - | 5.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 500 kwa kutumia bomba za HDPE 32mm (PN 10) huko Kitopeni ifikapo Juni 2025 | - | - | 5.00 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa kilomita 1 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) lenye kipenyo cha milimita 32 huko Kwemishuza ifikapo Juni 2023 | 9.00 | - | - |

| Na. | Maelezo | Gharama (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa kilomita 1 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) zenye kipenyo cha milimita 32 huko Sinza ifikapo Juni 2024 | - | 9.00 | - |
| | Kubadilisha mtandao wa bomba wenye urefu wa kilomita 1 kwa kutumia bomba za HDPE (PN 10) wenye kipenyo cha milimita 32mm, ifikapo Masaule Juni 2025 | - | - | 9.00 |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Maguzoni lenye mita za ujazo 225 | 5.00 | - | - |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Maguzoni lenye mita za ujazo 12 | 4.00 | - | - |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Kialilo ifikapo Juni 2024 | - | 3.00 | - |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Mbula ifikapo Juni 2023 | 3.00 | - | - |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Jegestali 1 ifikapo Juni 2025 | - | - | 6.00 |
| | Ukarabati wa ukuta wa ndani na nje wa tanki la kuhifadhia maji la Jegestali 2 ifikapo Juni 2025 | - | - | 6.00 |
| | Kuanza ujenzi wa tanki jipya la kuhifadhia maji lenye uwezo wa mita za ujazo 50 kuchukua nafasi ya tanki la Kipembe lenye ujazo wa mita za ujazo 12 ifikapo Juni 2025 | - | - | 15.00 |
| | Kununua na kufunga mita kubwa za kutenganisha maeneo ya kanda 10(DMA) (mita 3 katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, mita 3 katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 na 4 katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25) | 6.00 | 6.00 | 8.00 |
| | Kununua na kubadilisha valvu 20 za zilizochakaa. Valvu 10 kwa kila FY 2023/24 na 2024/25 | - | 5.00 | 5.00 |
| | Kununua na kufunga mita mpya kwa maunganisho 700 ya wateja ambao hawana mita za maji ifikapo Juni 2023 | 77.00 | - | - |
| | Kununua na kufunga mita za malipo kabla kwa wateja 52 wasio na mita ifikapo Juni 2024, mita 26 kwa mwaka | - | 10.4 | 10.4 |
| | Kununua na kubadilisha mita za maji 552 ifikapo Juni 2023 | - | 30.36 | 32.00 |
| | Kujenga mtambo wa kusafisha maji Magamba ifikapo Juni 2023 | 85.79 | - | - |
| | Kuweka paa kwenye matanki ya kuhifadhia na kuweka dawa za kuua vimelea kwenye matanki ya Maguzoni, Mbula na Jegestal | 3.00 | - | - |
| | Kununua zana za kufanya kazi pamoja na vifaa vya mabomba kama spana | 10.00 | 12.00 | 15.00 |
| | Kununua na kubadilisha viti 5 vya ofisi ifikapo Juni 2023 | 1.00 | - | - |
| | Kununua na kubadilisha meza 5 za ofisi ifikapo Juni 2023 | 2.50 | - | - |
| | Kununua na kubadilisha kabati 3 za faili ifikapo Juni 2023 | 3.00 | - | - |
| | Kununua na kubadilisha kompyuta 2 za ofisi ifikapo Juni 2023 | 6.00 | - | - |
| | Kununua pikipiki kumi na mbili (12) kwa shughuli za kiufundi (pikipiki 4 katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23, pikipiki 4 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 na pikipiki 4 | 16.00 | 16.00 | 16.00 |

| Na. | Maelezo | Gharama (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| | katika Mwaka wa Fedha 2024/25) | | | |
| | Kununua kompyuta 4 mpya kwa shughuli za anakara ya maji ifikapo Juni 2023 | 12.00 | - | - |
| | Kununua printa 2 mpya kwa kazi za ofisi ifikapo Juni 2024 | 1.50 | 1.50 | - |
| | Kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka ifikapo Juni 2025 | - | 25.00 | 25.00 |
| | Kununua na kufunga mita za maji kwa wateja wapya (mita 300 mwaka wa fedha 2022/23, mita 450 mwaka wa fedha 2023/24 na mita 450 mwaka wa fedha 2024/25) | 33.00 | 51.38 | 53.33 |
| | Kununua simu janja 8 kwa wasoma mita ifikapo Juni 2025 | 1.80 | 0.30 | 0.30 |
| | Jumla | 336.59 | 404.47 | 462.61 |

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(i))*

---

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Maunganisho Mapya ya Majisafi | No. | 300 | 450 | 450 |
| Upotevu wa Maji | % | 40 | 35 | 30 |
| Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato | % | 87 | 92 | 95 |

Dodoma, ........., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*